# UJANA SALAMA: MPANGO WA NYONGEZA YA FEDHA (CASH PLUS) UNAOHUSU USTAWI NA MABADILIKO SALAMA KWA VIJANA – MATOKEO YA MZUNGUKO WA3 TATHIMINI

## UTANGULIZI

Mradi wa nyongeza ya fedha "Cash plus' wa majaribio unaohusu Ustawi na Mabadiliko Salama kwa Vijana unaotekelezwa Tanzania, kwa kifupi "Ujana Salama", unalenga kuimarisha maisha ya vijana wa vijijini. Vijana hawa kutoka kaya maskini wanakabiliwa na changamoto nyingi za kiafya na kiuchumi, zikiwemo kukatisha masomo shuleni, mimba za utotoni, maradhi yaambukizwayo kwa njia ya ngono, ukatili, unyanyasaji na unyonyaji.[1]

Mradi huu wa Ujana Salama unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (Tanzania Social Action Fund (TASAF III)) na kuendeshwa kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (Productive Social Safety Net (PSSN)), unawalenga vijana wa umri wa balehe katika kaya za walengwa ambapo sambamba na uhawilishaji fedha vijana wanajengewa uwezo wa stadi za kazi na maisha (hafua zinazotolewa ni pamoja na katika wilaya nne za mikoa miwili ya Iringa na Mbeya. Katika utekelezaji wa Mpango huu utaalamu unatolewa na UNICEF Tanzania na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS). Tathmini ya mradi huu wa majaribio inatekelezwa na Ofisi ya Utafiti ya UNICEF – Innocenti, Chuo Kikuu cha Buffalo (State University of New York) na EDI Global, kwa kushirikiana na TASAF, TACAIDS na UNICEF Tanzania.

Mipango ya kinga ya jamii, ikiwa ni pamoja na uhawilishaji fedha, unazidi kutambuliwa kama njia muhimu ya kuwekeza kwa vijana wa umri wa balehe ili kuhakikisha wanakuja kuwa watu wazima wenye mafanikio na Afya. Kwa hiyo, kuwekeza katika vijana kuna matokeo muhimu katika kupunguza umaskini wa kurithi na kuleta ukuaji wa kiuchumi, hasa pale unapounganishwa na Mipango mingine ya kinga ya jamii, kama vile uendelezaji miundombinu na ukuzaji wa nafasi za ajira.

Mradi wa Ujana Salama unathibitishwa na ushahidi kwamba uhawilishaji fedha unaweza kuleta matokeo chanya kwa ustawi wa vijana. Hata hivyo, ikiwa peke yake, ni nadra kuweza kutatua changamoto zote zinazowakabili vijana wa umri wa balehe.[2] Kutatua vikwazo hivi, mradi wa Ujana Salama unatumia mafanikio ya PSSN na programu za nyongeza, zikiwemo mafunzo na uimarishaji wa mtandao wa rufaa na huduma za afya. Lengo la programu hii ya 'Cash Plus' ni kuwezesha ukuaji salama, bora na wenye tija kuelekea kwenye utu uzima na wakati huo huo kuimarisha uwezo wa serikali za mitaa/vijiji kupanga, kuratibu na kusimamia huduma zinazohusiana na afya, kujikimu na




Credit: © UNICEF/Rikke Le Kirkegaard

Maelezo ya picha: Kijana kutoka kaya ya walengwa wa Mpango wa kunusuru kaya Maskini akishiriki katika uzinduzi rasmi wa Mpango wa nyongeza ya fedha 'Cash Plus' wa Tanzania unaohusu ustawi na mabadiliko salama kwa vijana (jijini Mbeya, Septemba 2017)

1 PSSN Youth Study Evaluation Team, *Tanzania Youth Study of the Productive Social Safety Net (PSSN) Impact Evaluation: Endline Report,* UNICEF Office of Research—Innocenti, Florence, Italy, 2018.

2 Watson, C. and Palermo, T., *Options for a "Cash Plus" Intervention to Enhance Adolescent Well-being in Tanzania: An introduction and review of the evidence from different programme models in Eastern and Southern Africa,* UNICEF, Dar es Salaam, Tanzania, 2016.

kinga ya jamii. Uunganishwaji huu wa uhawilishaji fedha na programu za utoaji hafua zingine za kinga ya jamii ndiyo unajulikana kama mpango wa nyongeza ya fedha "Cash Plus".

## UJANA SALAMA: PROGRAMU YA CASH PLUS

Mradi wa Ujana Salama ulilengwa kwa vijana wa umri wa balehe wenye miaka 14–19 (katika utafiti wa mwanzo) katika kaya zinazonufaika na mpango wa Kunusuru Kaya Maskini na una vipengele vikuu vitatu:

1. Mafunzo ya vijana kwa ajili ya kujiendeleza kimaisha yanayojumuisha stadi za maisha, afya ya uzazi na ujinsia, UKIMWI (SRH-HIV) na mbinu za kujikinga na ukatili wa kijinsia.
2. Mafunzo ya vitendo (kuhusu njia mbadala za kuendesha maisha na kukabili matatizo) na ruzuku ya uzalishaji mali itakayotumika kwa ajili ya shule, vyuo vya ufundi, au mipango ya biashara; na,
3. Kuimarisha vituo vya afya na mtandao wa huduma rafiki kwa vijana za VVU, afya ya uzazi na ujinsia, na athari zinazotokana na vitendo vya ukatili.

Maeneo mawili ya Mamlaka ya utelekezaji wa Mpango wa TASAF yalichaguliwa ili kutekeleza mradi wa Ujana Salama, hii ilitokana na kuwepo kwa mpango wa kuzinusuru kaya maskini katika maeneo hayo lakini pia UNICEF walikuwa wakisaidia programu zingine katika maeneo hayo.[3] Maeneo haya ni katika halmashauri nne Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania: Mufindi na Mafinga katika Mkoa wa Iringa; Rungwe na Busokelo mkoani Mbeya.

Ratiba ya utekelezaji wa mradi ilikuwa kama ifuatavyo:

- **Januari – Mei 2018:** Mafunzo ya ana kwa ana na vijana wa umri wa balehe yaliyotolewa kwa majuma 12 *(tazama Jedwali la 1 kwa mada zilizofundishwa)*.
- **Juni 2018 – Machi 2019:** Mafunzo kwa vitendo kutoa msaada, kutia hamasa na kutoa mwongozo katika mipango ya kielimu na kibiashara.
- **Julai 2018:** Kuimarisha vituo vya afya kulikofanywa sambamba na uimarishwaji wa mitandao ya rufaa na kuunganishiwa kwa huduma rafiki kwa vijana zilizowezeshwa katika awamu yote ya mafunzo kwa vitendo.
- **Machi na Juni 2019:** Ruzuku za uzalishaji mali (sawa na Dola za Marekani 80) zilitolewa katika mkupuo mmoja au miwili baada ya kupokea mipango ya kielimu au kibiashara iliyoandaliwa na vijana.

## TATHMINI

Tathmini inatumia muundo wa majaribio wa kuchagua sampuli kwa kutumia njia ya bahati nasibu (RCT), ambapo vijiji 130 (vilichaguliwa bila mpangilio maalumu na kuwekwa katika makundi mawili ya utafiti:

1. utekelezaji wa afua za majaribio: Vijiji vinavyopokea fedha za PSSN pamoja na mradi wa Ujana Salama;
2. vijiji vya Mlinganisho: vijiji vinavyopata pesa katika Mpango wa kunusuru kaya maskinipeke yake.

Huu ni utafiti unaopima matokeo ya muda mrefu ukiwa na njia mchanganyiko, zikiwemo tatmini za awali (2017), ya Awamu ya 2 (2018) Awamu ya 3 (2019), na Awamu ya 4 (inayofanyika mwaka 2021).[4] Tathminiziliendeshwa katika vituo vya afya, kwenye kwa walengwa katika jamii, na watoa huduma pamoja na vijana wa umri wa balehe.

Taarifa hii inatoa muhtasari wa matokeo ya tathiminya taarifa zilizokusanywa katika awamu ya tatu, iliyofanyika miezi 26–28 baada ya tathmini ya mwanzo, mwaka mmoja baada ya mafunzo ya ana kwa ana, na mwezi mmoja hadi miwili baada ya uhawilishaji wa fedha. Kati ya tathminiya pili na awamu ya 3, yalianzishwa mafunzo kwa vitendo na uimarishaji wa mitazamo rafiki kwa vijana wanaobalehe kuhusu huduma za afya.

Hojaji za utafiti wa kitakwimu kwa ajili ya vijana zinagusa mada mbalimbali kutokana na nadharia ya mabadiliko, kama inavyoelezwa katika ripoti ya tathmini ya mwanzo (Awamu ya 1). Yanajumuisha matokeo ya hatua ya kati

3 Kwa sababu za kiutawala, TASAF inagusa maeneo ya kijiografia ya utekelezaji wa programu kama Mradi wa Mamlaka ya Kieneo (PAAs). Kwa upande wa Tanzania Bara, hizi ni sawa na halmashauri za serikali za mitaa. Kisha ndani ya PAAs, haya ni kata, vijiji/mitaa (mitaa ni eneo la utawala maeneo ya mijini, sawa na vijiji huko vijijini).

4 Njia ya utafiti kwa kutumia makundi mawili tofauti ilifanyika mwaka 2017, baada ya utekelezaji wa utafiti wa mwanzo, na iligawanywa kwa PAA na vijiiji (vijiji vikubwa dhidi ya vidogo).

(maarifa, mitizamo na hamasa) na matokeo ya muda wa kati hadi mrefu (mabadiliko ya kitabia na matumizi ya huduma za afya).

Kwa upande wa uchambuzi wa utafiti wa kitakwimu, tulitumia data kutoka +kundi la mlinganisho la vijana wa balehe katika vijiji vya mradi na vile vya mlinganisho na kulinganisha mabadiliko ndani ya kipindi fulani kati ya makundi hayo mawili. Kwa upande wa uchambuzi wa utafiti wa maelezo, tulifafiti mbinu na njia mbalimbali ili kuchunguza athari kupitia mahojiano kwa kina kwa kutumia kundi dogo la vijana wa balehe 32 katika mikondo yote mitatu.

**Jedwali la 1:** ***Mada za mafunzo***

### UJASIRIAMALI

- Ndoto na malengo
- Stadi za ujasiriamali
- Mipango ya biashara na utunzaji kumbukumbu
- Uwekaji akiba
- Wajibu wa mjasiriamali

### VVU & AFYA YA UZAZI NAJINSIA

- Kuvuka salama kipindi cha balehe
- Mahusiano
- Elimu, kuzuia na kinga ya VVU
- Kujiweka kwenye hatari kingono na kinga
- Mimba na uzazi wa mpango
- Ukatili na ukatili wa kijinsia
- Kutatua mitazamo hasi na kaida za jinsia
- Vileo na dawa za kulevya
- kanuni za afya na lishe

Wakati wa kutafsiri matokeo ya Awamu ya 3, kulikuwa na vigezo vitatu vya kuzingatia. Kwanza, kaya zilikabiliwa na ucheleweshaji wa uhawilishaji ruzuku kwa awamu mbili ambapo Mpango wa kunusuru hutoa ruzuku kila baada ya miezi mwili, hii ikiwa ni mara ya kwanza tangu kuanza kwa mradi huu wa kusaidia kaya maskini mwaka 2015, na jambo hili lilitokea muda mfupi kabla TAKWIMU za Awamu ya 3 hazijakusanywa. Kaya zilipokea malipo yao kamili ya mwisho mwezi wa Machi, 2019 na baadaye zilipaswa kupata malipo mengine mwezi Mei 2019, lakini hilo halikutokea. Hakukuwa na malipo mengine ya nyongeza wakati ukusanyaji wa taarifa ulipofika mwisho (Agosti, 2019). Huenda hii ilipunguza uwezekano wa manufaa ya mradi wa uhawilishaji fedha, kwani kaya zilimudu kukosekana huku kusikotarajiwa kwa kipato cha kila mara. Pili, ruzuku za uzalishaji mali zililitolewa muda mfupi kabla ya taarifa za Awamu ya 3 kukusanywa, kwa hiyo huenda matokeo kamili yalilikuwa bado kuonekana bayana au, huenda baadhi ya vijana hawakuwa wamepokea fedha za ruzuku wakati walipohojiwa. Tatu, tathmini hii ilichunguza matokeo kwa upana mkubwa (tazama Jedwali la 2), ikiashiria michango ya juhudi hii ilitoka katika sekta nyingi huku vijana wa umri wa balehe wakikabiliwa na hatari za aina nyingi wanazokabiliana nazo vijana katika kipindi cha balehe. Athari kubwa za Mradihazikutarajiwa kwenye matokeo yote katika awamu hii.

## MATOKEO YA AWAMU YA 2

Ripoti ya Awamu ya 2 ya utafiti ilionyesha kwamba, katika tatmini ya kati, baada ya vijana wa umri wa balehe walikuwa wameshapata mafunzo ya ana kwa ana ya majuma 12, yalipatikana matokeo chanya kuhusu ushiriki katika shughuli za kiuchumi, mitazamo chanya kuhusu jinsia, na maarifa kuhusu VVU na Afya ya Uzazi

**Jedwali la 2:** ***Tathmini ya matokeo***

### MATOKEO YA MUDA MFUPI

- Vivutio vya kielimu na kujishughulisha kikazi
- Mitazamo chanya ya usawa wa kijinsia
- Elimu ya njia za kisasa za uzazi wa mpango
- Elimu ya kuzuia VVU
- Elimu kuhusu pahali pa kutafuta huduma za SRH/ VVU na msaada dhidi ya ukatili

### MATOKEO YA MUDA WA KATI NA MREFU

- Fursa za ajira kwa vijana na shughuli za kujiingizia kipato
- Mafanikio katika elimu na mafunzo
- Kujenga uwezo zaidi wa kutafuta huduma sahihi za SRH/VVU na mwitikio dhidi ya ukatili
- Kuchelewesha umri wa  kuanza kushiriki ngono, ndoa za utotoni na mimba za utotoni
- Kupungua kwa ushiriki katika uhusiano wenye ukatili wa kingono na tabia zinazoleta hatari ya VVU
- Kuimarika kwa afya ya akili
- Kupungua kwa matukio ya watu kuathirika na vitendo vya ukatili

na ujinsia. Hata hivyo, hakukuwa na matokeo juu ya vitendo vya ukatili, tabia hatarishi za VVU, au kuimarika kwa tabia ya kutafuta huduma za Afya ya Uzazi na jinsia na VVU. Matokeo haya yalionyesha ni jinsi gani, mara baada ya mafunzo, huenda vijana wa balehe walikuwa wamekwishaanza kupata maarifa na kufikiria kuhusu maisha yao ya baadae kwa njia tofauti. Hata hivyo, kujihusisha kwao na mradi huu katika Awamu ya 2 ulikuwa mfupi kiasi na wakati huohuo, vipengele vingine (kuimarisha mafunzo kwa vitendo, rusuku na uimarishaji wa rufaa na mitandao ya huduma) vilikuwa bado havijaanza. Pia, kuna dhana kwamba matokeo haya ya kitabia yangalichukua muda zaidi kutokea na huenda zingalionekana katika Awamu ya 3 ikiwa kweli programu ilikuwa ndiyo sababu ya matokeo hayo.

## MATOKEO YA AWAMU YA 3

Matokeo ya Awamu ya 3 yalionyesha kuongezeka kwa utoaji wa huduma rafiki kwa vijana wa umri wa balehe katika vituo vya afya, na pia matokeo chanya katika: ufahamu wa Afya ya Uzazi na ujinsia na VVU; mitazamo ya usawa wa kijinsia; uwezekano wa mtu kuanzisha biashara; muda uliotumika katika ufugaji; afya ya akili; mitazamo ya kijasiriamali; kujiamini; upimaji wa VVU; na ziara katika vituo vya afya. Athari chanya za nyongeza za kujikinga zilionekana, zikiwemo kupungua kwa ukatili wa kingono na kimwili na kuchelewa katika kuanza kushiriki ngono. Hata hivyo, vilevile tuliona kuna kupungua kwa mahudhurio katika shule za sekondari, hasa kwa wasichana wa umri wa balehe.

**Hamasa za kielimu, ushiriki katika shughuli za kiuchumi**

- Vijana waliokuwa sehemu ya mradi walikuwa na uwezekano mkubwa wa kuanzisha biashara ndani ya mwaka mmoja uliopita na kutumia muda wao zaidi katika ufugaji.
- Mradi haukupunguza uwezekano wa vijana kupatwa na hatari katika kazi, wala haukuathiri taarifa za kujeruhiwa au ugonjwa.
- Ushiriki wa vijana katika majukumu ya nyumbani haukuathirika.
- Mradi haukuwa na athari katika kiwango cha elimu (darasa la juu zaidi lililofikiwa) wala kama mtu amehitimu elimu ya msingi.
- Kulikuwa na kushuka kwa idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari kutokana na kukatisha masomo miongoni mwa kundi dogo la utafiti la wasichana. Kabla ya mradi kuanza, wasichana walikuwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kuhudhuria elimu ya sekondari kuliko wavulana. Vilevile, wasichana walikuwa na kiwango cha juu cha ushiriki katika programu ya mafunzo ya 'cash plus'. Mambo haya huenda yalichangia katika athari zilizoonekana kwa wasichana. Kwa kiasi kikubwa, ukatishaji masomo ulitokea kabla ya malipo ya ruzuku, jambo linaloashiria kwamba huenda vijana walikuwa wameamua kukatisha masomo wakati wa mafunzo au muda mfupi baadae, pengine wakitumaini kupata kipato kutokana na ruzuku au kipato kutoka kwenye biashara. Masuala ya kimuktadha, ikiwemo kukosekana kwa fursa za kazi kwa vijana walioelimika, huenda pia yalichangia.

**Masuala ya VVU, SRH na uungwaji wa huduma**

- Mradi huu umesaidia umri wa wasichana kuanza kujihusisha na ngono kuongezeka kwa takribani kwa miezi minne hivi.
- Hakukuwa na athari katika ndoa/kuishi pamoja kama mke na mume wala uwezekano kuwa vijana balehe walikuwa na wapenzi.
- Mradi huu uliongeza ufahamu kuhusu njia za kisasa za kuzuia mimba.
- Mradi huu uliongeza ufahamu kuhusu kuzuia VVU kwa asilimia 5.2.
- Hakukuwa na matokeo katika hatari ya VVU iliyodhaniwa.
- Mradi uliongeza upimaji wa VVU katika miezi 12 iliyotangulia kwa asilimia 6.3.
- Kwa vijana wa balehe waliojizuia kuanza kushiriki ngono, hakukuwa na matokeo kwa ngono ya kubadilishana.
- Mradi uliongeza utafutaji huduma katika vituo vya afya, kwa upande wa wavulana.
- Taratibu, vituo vya afya vimekuwa sehemu rafiki kwa vijana wa umri wa balehe, kulinganisha na Awamu za 1 na 2.
- Matokeo chanya ya ongezeko la kutafuta huduma katika vituo vya afya, ubora wa huduma, na ufahamu kuhusu pahali pa kupata huduma

inaashiria kuimarika kwa upande wa utoaji huduma na uunganishwaji na huduma hizi kama sehemu ya mradi.

**Kupungua kwa vitendo vya ukatili**

- Mradi wa 'cash plus' ulipunguza matukio ya ukatili wa kingono katika miezi 12 iliyokuwa imetangulia kwa asilimia 3.7.
- Mradi ulipunguza matukio ya ukatili wa kimwili kwa asilimia 3.3 (kushuka wa matukio ya ukatili kwa asilimia 47.8), kwa msukumo wa wanaume.
- Hakukuwa na matokeo yoyote katika masuala ya ukatili wa kihisia na kimwili.
- Hakukuwa na matokeo katika viashiria vya utoaji taarifa za ukatili (kuomba msaada).

**Usawa wa jinsia, afya ya akili na mitazamo mbalimbali**

- Mradi ulipunguza dalili za sonona lakini hakukuwa na mabadiliko katika msongo na namna mtu alivyojidhania.
- Mahojiano ya kina yalionyesha jinsi hali tete za kiuchumi zinavyochangia katika msongo wa mawazo unaotokana na ukosefu wa usalama wa chakula, mahitaji muhimu na kulipia vifaa vya shule, hata miongoni mwa kundi la wagonjwa.
- Mradi uliongeza fikra za kijasiriamali na kujiamini.
- Mradi uliongeza mitazamo ya usawa wa jinsia, hasa katika kazi za nyumbani na maisha ya kila siku.

## HITIMISHO

Mradi wa 'Ujana Salama' unalenga kutumia matokeo ya uhawilishaji fedha yakifanywa pamoja kutoa mafunzo kwa vijana ya namna ya kuendesha maisha na Afya ya Uzazi najinsia/VVU, mafunzo kwa vitendo na ruzuku za uzalishaji mali na pia uunganishwaji na huduma rafiki kwa vijana wa balehe za Afya ya Uzazi na jinsia/VVU.

Wakati wa tathmini ya pili, mara baada ya mafunzo ya ujasiriamali na Afya ya Uzazi na ujinsia, ilibainika kuwa mradi ulikuwa na matokeo chanya kwenye viashiria vya muda mfupi, kama vile elimu ya Afya ya Uzazi na jinsia, mitizamo chanya ya jinsia na ushiriki katika shughuli za kiuchumi. Mwaka mmoja baadae, na baada ya vijana wa umri wa balehe kuwa wamefundishwa kwa vitendo, tuligundua mabadiliko ya tabia kwa kiasi fulani, ikiwemo: ongezeko la upimaji VVU na watu kwenda katika vituo vya afya kwa wingi zaidi; kuongezeka kwa umri wa kuanza kushiriki ngono; kupungua kwa utokeaji na vitendo vya ukatili; kuimarika kwa hali ya kujiamini na mitazamo ya kijasiriamali kujengeka; na kupungua kwa dalili za sonona. Katika maeneo mengine hakukuwa na mabadiliko na kwa upande wa mahudhurio shuleni kulikuwa na athari hasi kwa kiasi fulani.

Mafunzo ya kuimarisha njia za kujiendeshea maisha yalikuza ari ya ujasiriamali, kujiamini na umiliki wa biashara. Maeneo ya vijijini Tanzania, fursa za uzalishaji ni haba na mara nyingi huishia katika kilimo cha kujikimu tu, biashara ndogondogo, au kufanya kazi katika mashamba makubwa ya mazao ya biashara. Tija inayopatikana katika mfumo wa elimu inaweza kuchukuliwa kuwa iko chini, jambo ambalo huenda liliathiri uamuzi miongoni mwa vijana ili kupata elimu, hii ni kwa vijana waliokuwa na mbadala wa namna ya kujiendeshea maisha kwa sababu ya mradi wa cash plus.

Uwezo wa huduma za afya uliimarika, ikiwemo kuzuia VVU na elimu ya njia za uzazi wa mpango, upimaji wa VVU na kutafuta huduma katika vituo vya afya kwa uchunguzi. Kulikuwa na kuimarika katika mitazamo ya usawa wa jinsia na kupungua kwa ukatili wa kingono na utokeaji wa vitendo vya ukatili wa kimwili. Matokeo ya utafiti huu yana umuhimu mkubwa. Mradi huu wa cash plus huenda ukasaidia kuvunja urithi wa ukatili wa kizazi hadi kizazi, kwani taratibu za aina hiyo hupokelewa wakati wa balehe na mitazamo hiyo kuimarishwa kipindi hicho. Watoto wanaoshuhudia vitendo vichache vya ukatili katika familia zao watakua watu ambao hawatatumia ukatili sana dhidi ya wenzi wao wa maisha.

Mapendekezo kwa uandaaji wa mradi na tafiti kwasiku zijazo yanajumuisha umuhimu wa kutilia mkazo wa mafunzo katika kuanzisha biashara badala yake kusisitiza umuhimu wa elimu na fursa za mafunzo ya ufundi na uanagenzi. Kuna haja ya kuendelea kuimarisha mtandao wa rufaa na uunganishaji wa huduma za VVU na afya ya uzazi na ujinsia kwa vijana wa umri wa balehe na kuimarisha uelewa wa vijana kuhusu hatari za maambukizi ya VVU. Zaidi ya hayo, licha ya kupita muda mfupi kiasi fulani tangu kutolewa kwa ruzuku za uzalishaji mali na ukusanyaji wa data katika Awamu ya 3, sampuli iliyochaguliwa ifuatiliwe zaidi ili kuelewa matokeo kamilifu ya ruzuku katika elimu/mafunzo ya ufundi na matokeo ya kiuchumi, na pia kufanya mafanikio ya programu kuwa endelevu.

Utafiti huu ndio wa kwanza kuonyesha ushahidi wa ufanisi wa mradi wa nyongeza ya fedha “cash plus” **uliotekelezwa ndani ya mradi unaoendelea wa serikali wa kusaidia kaya maskini.** Katika kipindi hiki ambapo dunia inashuhudia idadi kubwaya vijana walio kwenye umri wa balehe, ni muhimu kuelewa njia na uwekezaji upi vikitumika pamoja zinaweza kusaidia ukuaji salama, ili kujenga hatma njema kwa kizazi hiki na watoto wao. Utafiti huu unatoa ushahidi madhubuti wa kuelewa namna gani cash plus inaweza kuwasaidia vijana kukua kwa usalama hadi utu uzima nchini Tanzania, Afrika na duniani kote.

Muhtasari huu umeandikwa na Timu ya Tathmini ya Mradi wa Cash Plus kwa Vijana wa Balehe Tanzania (“Tanzania Adolescent Cash Plus Evaluation Team”). Ofisi ya Utafiti ya UNICEF—Innocenti: Valeria Groppo, Jacobus de Hoop, Lusajo Kajula, Leah Prencipe, Jennifer Waidler. Chuo Kikuu cha Buffalo: Tia Palermo (Mchunguzi Mkuu Mwenzi). EDI Global: Johanna Choumert Nkolo (Mchunguzi Mkuu Mwenzi), Respichius Mitti (Mchunguzi Mkuu Mwenzi), Nathan Sivewright, Koen Leuveld, Bhoke Munanka. TASAF: Paul Luchemba, Tumpe Lukongo. TACAIDS: Aroldia Mulokozi. UNICEF Tanzania: Ulrike Gilbert, Paul Quarles van Ufford, Rikke Le Kirkegaard, Frank Eetaama.

Ufadhili wa mradi huu wa majaribio na tathmini umetolewa na Oak Foundation na UNICEF. Fedha za nyongeza kwa ajili ya tathmini ilitolewa na DFID na Sida kupitia Ofisi ya Utafiti ya UNICEF ya misaada ya fedha—Innocenti ikisaidia Mradi wa Transfer. Fedha zaidi kwa utekelezaji wa shughuli zilitolewa na Irish Aid.

Kwa taarifa zaidi kuhusu programu na matokeo ya utafiti wa kati, soma ripoti kamili full report: Timu ya Tathmini ya Mradi wa Cash Plus kwa Vijana wa Balehe Tanzania, Modeli ya ‘Cash Plus’ kwa Ukuaji Salama kuingia katika Utu uzima Bora na wenye Tija: Ripoti ya Utafiti Awamu ya 3 (Tanzania Adolescent Cash Plus Evaluation Team, A Cash Plus Model for Safe Transitions to a Healthy and Productive Adulthood: Round 3 Report), Ofisi ya Utafiti ya UNICEF—Innocenti, Florence, 2020.Adulthood: Round 3 Report, UNICEF Office of Research—Innocenti, Florence, 2020.

The Office of Research – Innocenti is UNICEF’s dedicated research centre. It undertakes research on emerging or current issues in order to inform the strategic directions, policies and programmes of UNICEF and its partners, shape global debates on child rights and development, and inform the global research and policy agenda for all children, and particularly for the most vulnerable. The views expressed are those of the authors and/or editors. For rights of reproduction or translation, apply to UNICEF Office of Research – Innocenti. Short extracts may be reproduced unaltered without authorization on condition that the source is indicated. © UNICEF Office of Research

**UNICEF OFFICE OF RESEARCH-INNOCENTI**
Florence, Italy

www.unicef-irc.org

+39 055 20330

florence@unicef.org
@UNICEFInnocenti
facebook.com/UnicefInnocenti

**For every child, answers**